

*Sheria Ndogo (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 195 la tarehe 11/06/2004

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),  
1982

(NA. 7 YA 1982)

---

**SHERIA NDOGO**

---

*Imetungwa chini ya Kifungu cha 148*

---

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE, 2004

Jina 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (kuanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii), Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, 2004.

Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi tasfiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-

Namba 7  
ya mwaka  
1982 "Bodi" maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoungwa chini ya sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982;

"Kadi " maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama;

"Halmashauri " maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe;

"mchango" maana yake ni mchango wa hiari, utakaotolewa na mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Mganga Mkuu wa Wilaya" maana yake ni daktari ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za huduma za afya wilayani;

"huduma za afya " maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na hospitali za serikali na watu binafsi; na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na vituo vya afya na zahanati;